**MSWADA WA KATIBA YA KENYA (MAREKEBISHO), 2025**

**Mswada wa**

**SHERIA ya kurekebisha Katiba ya Kenya**

**IMEPITISHWA** na Bunge la Kenya ifuatavyo—

Anwani fupi.

**1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Katiba ya Kenya (Marekebisho), 2025.

Uchopekaji wa Ibara mpya kwenye Katiba.

**2.** Katiba imerekebishwa kwa kuchopeka Ibara mpya zifuatazo baada tu ya Ibara ya 204 –

Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Maeneobunge.

**204A.** (1) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Maeneobunge imeundwa.

(2) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Maeneobunge imeundwa ili kuhakikisha utekelezaji wa majukumu mahususi ya Serikali ya Taifa katika kila eneobunge.

(3) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Maeneobunge ni hazina ya serikali ya taifa kutoka kwa mgao wa fedha uliotengewa serikali ya taifa kupitia kwa Sheria ya Kugawa Mapato ya kila mwaka ambayo hupitishwa kwa mujibu wa Ibara ya 218.

(4) Pesa zote zinazotengwa kwa mujibu wa Ibara hii zitachukuliwa kuwa fedha zilizotengewa maeneobunge na zitasimamiwa na kutumiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria.

(5) Bunge litapitisha sheria ya kuweka masharti zaidi ya utekelezaji wa Ibara hii.

Hazina ya Uangalizi ya Seneti.

**204B.** (1) Hazina ya Uangalizi ya Seneti imeundwa.

(2) Hazina ya Uangalizi ya Seneti imeundwa ili kuhakikisha kwamba Seneti ina rasilimali na imewezeshwa kikamilifu kutekeleza majukumu yake ya uangalizi.

(3) Hazina ya Uangalizi ya Seneti ni hazina ya serikali ya taifa kutoka kwa mgao wa fedha uliotengewa serikali ya taifa kupitia kwa Sheria ya Kugawa Mapato ya

kila mwaka ambayo hupitishwa kwa mujibu wa Ibara ya 218.

(4) Pesa zote zinazotengwa kwa mujibu wa Ibara hii zitachukuliwa kuwa fedha zilizotengewa Seneti na zitasimamiwa na kutumiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria.

(5) Bunge litapitisha sheria ya kuweka masharti zaidi ya utekelezaji wa Ibara hii.

Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Hatua Sawazishi.

**204C.** (1) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Hatua Sawazishi imeundwa.

(2) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Hatua Sawazishi imeundwa ili kuimarisha mikakati ya serikali ya taifa kuhusu hatua sawazishi.

(3) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Hatua Sawazishi ni hazina ya serikali ya taifa kutoka kwa mgao wa fedha uliotengewa serikali ya taifa kupitia kwa Sheria ya Kugawa Mapato ya kila mwaka ambayo hupitishwa kwa mujibu wa Ibara ya 218.

(4) Bunge litapitisha sheria ya kuweka masharti zaidi ya utekelezaji wa Ibara hii.

## MAELEZO YA MADHUMUNI NA SABABU

**Kauli ya madhumuni na sababu za Mswada**

Lengo kuu la Mswada huu ni kurekebisha Katiba ili kukita hazina zifuatazo katika Katiba—

(a) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Maeneobunge;
(b) Hazina ya Uangalizi ya Seneti; na
(c) Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Hatua Sawazishi.

Kukitwa kwa Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Maeneobunge kwenye Katiba kutahakikisha kwamba majukumu mahususi ya serikali ya taifa yanafikia maeneobunge yote kama inavyokusudiwa kwenye Ibara ya 6(3) ya Katiba na kutahakikisha ushirikishwaji wa umma katika utambuaji na utekelezaji wa mipango ya serikali ya taifa iliyopewa kipaumbele.

Kukitwa kwa Hazina ya Uangalizi ya Seneti kwenye Katiba kutahakikisha kwamba Seneti inawezeshwa na ina rasilimali na imewezeshwa kikamilifu kutekeleza majukumu yake ya uangalizi.

Kukitwa kwa Hazina ya Serikali ya Taifa kwa Hatua Sawazishi kwenye Katiba kutaimarisha mikakati ya serikali ya taifa kuhusu hatua sawazishi.

**Kauli ya ukasimishaji wa mamlaka ya kutunga sheria na udhibiti wa haki na uhuru wa kimsingi.**

Mswada huu haukasimishi mamlaka ya kutunga sheria wala haudhibiti haki na uhuru wowote wa kimsingi.

**Kauli iwapo Mswada unahusu serikali za kaunti**

Kwa mujibu wa Ibara 256 ya Katiba, Mswada wa kurekebisha Katiba unaoanzishwa na Bunge utashughulikiwa na Bunge la Taifa na Seneti.

**Kauli iwapo Mswada unahusu masuala ya fedha kwa mujibu wa Ibara ya 114 ya Katiba**

Mswada huu una vipengele vinavyohusu utengaji na utumiaji wa fedha za umma.

Tarehe…………………………………………….., 2025

**SAMUEL CHEPKONG'A,**
***Mbunge.***

**OTIENDE AMOLLO,**
***Mbunge.***